# JARIBIO LA MTIHANI WA SHULE
# DARASA LA TANO - MWAKA 2021
# KISWAHILI : LUGHA

SASON 007

5

***JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU***

1. *Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina Maswali 50*
2. *Hakikisha umeandika:-*

   ***(i) JINA LAKO*** ***(ii) JINA LA SHULE YAKO***

**Muda: Saa 1 Dk. 40**

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi, umepewa maneno manne hapo chini. Chagua neno lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa;***

Siku ___1___ Linda na wazazi ___2___ walienda kutembelea sehemu za makao ___3___ wanyama wa pori. Ilikuwa siku ya Jumamosi, Linda ___4___ wazazi ___5___ walipoanza safari. Jumapili wakafika mahali ___6___ kulikuwa na wanyama ___7___ aina ___8___. Mifano ya wanyama ___9___ ni nguruwe mwitu, swala, nyati na tumbili.

Tumbili ni ___10___ mtundu sana ___11___ hupenda kuchezea watu. Linda alikuwa na ___12___ ya soda mkononi. Tumbili naye alikuwa kando ___13___ ya mti. Akashuka polepole akampokonya ___14___ mtoto chupa ya soda ___15___ kutoroka.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. mmoja | B. moja | C. kimoja | D. wamoja |
| 2. | A. yake | B. chake | C. wake | D. mwake |
| 3. | A. ya | B. lake | C. nake | D. huu |
| 4. | A. cha | B. lao | C. nao | D. na |
| 5. | A. wao | B. wake | C. wako | D. wa |
| 6. | A. hicho | B. hao | C. hapo | D. hivyo |
| 7. | A. wa | B. ya | C. cha | D. za |
| 8. | A. nyingine | B. wa | C. kingi | D. nyingi |
| 9. | A. huyo | B. mwingi | C. hao | D. chao |
| 10. | A. mnyama | B. wanyama | C. kinyama | D. unyama |
| 11. | A. wewe | B. yeye | C. mnyama | D. wao |
| 12. | A. vyumba | B. wingi | C. nyupa | D. chupa |
| 13. | A. ndani | B. vyupa | C. juu | D. ndani |
| 14. | A. yule | B. dani | C. kile | D. vile |
| 15. | A. na | B. nao | C. wa | D. kwa |

***Kutoka swali la 16 - 30, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa;.***

**16.** Nikikusaidia utaniambia ___________.

A. barikiwa B. ahsante
C. karibu D. sawa

**17.** Mmea wa mgomba huzaa ___________.

A. gomba B. migomba
C. ndizi D. pamba

**18.** Shati langu ni ___________ pepepe.

A. jeupe B. nyeupe
C. leupe D. mweupe

***Kanusha;***


**19.** Yeye anaoga kwa maji baridi.

A. Yeye anaoga kwa maji baridi.
B. Wao hawaoga kwa maji moto.
C. Yeye haogi kwa maji baridi.
D. Huyu anaoga maji baridi.

**20.** Wao walilia sana.

A. Wao hawakulia sana.
B. Huyu alicheka kidogo.
C. Huyo hakucheka sana.
D. Wao walifurahi kidogo.

**21.** Umbo hili huitwaje?



A. Pia B. Kopa
C. Hilali D. Jicho

**22.** Embe ___________ limeiva?

A. ipi B. yupi
C. ngapi D. lipi

***Andika kwa umoja;***

**23.** Hizo ni dawa za kulevya.

A. Hii ni dawa ya kulevya.
B. Hiyo ni madawa ya kulevya.
C. Huu ni dawa wa kulevya.
D. Hiyo ni dawa ya kulevya.

**24.** Nyuki hukaa kwenye ___________.

A. miti B. maua
C. mzinga D. nyumba

**25.** Kiti ___________ ni cha mtu mgani?

A. hiki B. hichi
C. hivyo D. yule

**26.** ***Kamilisha methali:-***

Polepole ndio ___________.

A. kufika B. kutochoka
C. mwendo D. kwao

**27.** ***Tumia -amba;***

Mkoba ___________ una uchafu ni huu.

A. ambazo B. ambao
C. ambayo D. ambamo

**28.** ***Kamilisha;***

Soko ________ mefungwa.

A. i B. zi
C. ya D. li

**29.** Jiko la makaa huitwaje?

A. Buli B. Seremala
C. Seredani D. Kinu

**30.** Malaria huambukizwa na ___________.

A. mbung'o B. nzi
C. umbu D. mbu

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31 - 40.***

Hapo zamani za kale palikuwa na ndugu watatu. Walipendana sana kama chanda na pete na pia walifanana kama shilingi kwa ya pili. Majina ya ndugu hawa watatu yalikuwa ni Jitupepo, Jitumaji na Jitumoto.

Jitupepo aliwasaidia ndugu zake kazi ya kupika. Alipenda kupika sana na chakula chake kilikuwa kitamu kama asali. Jitumaji alikuwa na kazi ya kuosha kila kitu na kufua nguo. Kila kitu kilikuwa safi kwa bidii ya Jitumaji. Alikuwa na bidii za mchwa.

Jitumoto alikuwa na kazi ya muhimu sana. Kila mtu alipata joto kwa sababu ya Jitumoto. Kila mtu alifurahia kazi ya ndugu yake.

31. Kulikuwa na ndugu wangapi?
A. Mmoja
B. Watatu
C. Watano
D. Wawili

32. Kazi ya kuosha ilifanywa na __________.
A. Jitumaji
B. Jitumoto
C. Wote
D. Jitupepo

33. ____________ alisaidia kwa kazi ya kupika.
A. Jitumoto
B. Jitumaji
C. Wote
D. Jitupepo

34. Ndugu hao ______________.
A. walisoma
B. walipigana
C. walipendana na kupigana
D. walipendana na kufanana

35. Ni nani alidumisha usafi?
A. Jitupepo
B. Jitumaji
C. Jitumoja
D. Jitupepo

36. Jitumoto alisaidia kuleta __________.
A. joto
B. moto
C. mvua
D. hewa

37. Kila mtu alifurahia _________ ya ndugu yake.
A. joto
B. hewa
C. kazi
D. maji

38. Ni nani kati ya hawa hajatajwa?
A. Jitumoja
B. Jitupepo
C. Jitumaji
D. Jitumoto

39. Ndugu hao walifanana kama __________.
A. chanda na pete
B. shilingi kwa ya pili
C. uta na upote
D. ulimi na mate

40. Hadithi hii ni juu ya ____________.
A. Jitumoto
B. Ndugu wengi
C. Jitupepo na hewa
D. Ndugu watatu

***Soma barua ifuatayo kisha ujibu maswali 41 - 50;***

Shule ya Msingi ya Tumaini,
S. L. P 4222,
Nyahururu.
Januari 28, 2021.

Kwa rafiki yangu Roda,

Salamu nyingi tele, nzito za heri, furaha na buraha kutoka kwangu. Nikitumai pia wewe u buheri wa afya. Madhumuni ya barua hii ni kutaka kujua jinsi unavyoendelea na masomo yako katika shule ya Manispaa.

Ningetaka kukujulisha kwamba shule yetu ina majengo mapya. Tuna jengo la ghorofa na pia kuna walimu wapya, mwalimu mkuu ni Bwana Mwaura, mwalimu wangu wa somo la jamii ni Bwana Githinji na Bi Maina ni mwalimu wangu wa sayansi.

Ni hayo tu kwa sasa ninakutakia kila la heri katika yote uyatendayo. Wasalimie rafiki zako na pia bibi na babu. Uwasalimie kila anayeniuliza.

Ni mimi wa chanda na pete,
Njoroge.

**41.** Mwandishi anasomea shule ya ________

A. upili B. kibinafsi
C. msingi D. ualimu

**42.** Barua hii iliandikwa muhula wa ________

A. pili B. kwanza
C. hakuna D. tatu

**43.** Barua hii ni mfano wa barua ya ________.

A. kupendana B. kirafiki
C. rasmi D. kishule

**44.** Ni walimu wangapi waliojiunga na shule hii?

A. Mmoja B. Hakuna
C. Mbili D. Watatu

**45.** Mwandishi wa barua hii anaitwa nani?

A. Mwaura B. Githinji
C. Njoroge D. Roda

**46.** Bwana Githinji na Bi. Maina ni ________

A. walimu B. marafiki
C. wanafunzi D. wazazi

**47.** Roda na Njoroge wote ni ________.

A. marafiki B. wavulana
C. watu D. watoto

**48.** Jina jingine la bibi ni ________.

A. amu B. shangazi
C. dada D. nyanya

**49.** Ni walimu wangapi wametajwa katika barua?

A. Watatu B. Wawili
C. Mmoja D. Wengi

**50.** Taja aina hiyo nyingine ya barua.

A. Barua nzuri
B. Barua rasmi
C. Barua ndugu
D. Barua